JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 442

Kwenyi meza ya duwara kisiasa mjini Kinshasa

# Bwana Birindwa kateuliwa waziri mkuu mpya

Kutokana na misukosuko ya kisiasa yaangamiza bado nchi ya Zaïre tangu hapo Raïs Mobutu kumuachisha bwana Tshisekedi madaraka ya uwaziri mkuu mwezi wa Ogusti 1992 ingawa kavikwa madaraka hayo na Mkutano mkuu wa kitaifa, uongozi wa nchi waonya kuwa waenda kinyume cha hatua nyingi kachukuliwa kwenyi mkutano huo muhimu na toka hayo siasa ya udemokrasia kufinywa. Kwani haijulikane kwa sasa nchi yaelekezwa wapi kutokana na vitendo vyafanywa na wanasiasa.

Kweli, baada ya Raïs Mobutu kuitisha mkutano wa wanasiasa na wengineo wawakilishi wa viungo mbalimbali vya kiraïa kwenyi meza ya duwara (table ronde) mnamo tarehe 9 marsi na baada ya kazi za tume mbalimbali kuundwa, wahuzuriaji kamteuwa kwa kauli moja bwana Faustino Birindwa kama vile waziri mkuu mpya atakaye unda serkali ya muungano mkubwa wa kiraïa muda huu wa mpito wabaki.

Katika maoni katoa bwana Birindwa baada ya kuchaguliwa, mheshimiwa huyo kanena kuwa ili mambo yaongoke haifai kutumika katika magonvi na ujeuri. Kuwa mbele ya kuunda serkali mpya yafaa kukutana na Raïs Mobutu katika masimulizi rasmi kuhusu hali iliyoko kwa sasa nchini. Ni hivi kakutana hapo majuzi na Mareshali Mobutu kunako mashua yake "Kamanyola".

Akiwanongonezea wapashahabari machache kasimulia na Raïs wa Jamhuri, bwana Birindwa kajulisha kuwa ili apate kutumika ginsi ifaavyo alimuomba Raïs amuache huru katika uongozi wa mambo yanayo elekea feza na uchumi wa nchi. Kwani yeye ni waziri katika mpito kwa kuitayarisha Jamhuri ya Tatu lakini hayupo waziri katika jamhuri ya Pili kaongozwa na chama kimoja tu. Bali aweza kumuona mara na mara Raïs wa Jamhuri kuhusu mambo yanayoelekea usalama, ukingo wa nchi, uhusiano na nchi za kigeni pia ; ili tusitumbukie tena katika makosa ya zamani.

Baadae atakutana na vikundi mbalimbali vya kisiasa na vingineo hasa kwanza "UDPS" ambamo abaki mwanachama na Umoja mtakatifu wenyi msimamo wa upinzani mkali. Akiendelea kujitetea bwana Birindwa kasema abaki mpinzani na hayupo katika upande wa Raïs wa Jamhuri. Bali kama vile waziri mkuu, serkali yake itahusika zaidi na usalama wa watu na mali zao. Na kwa hiyo yafaa kwanza kuchunguza hali ya askari-jeshi na wengineo wanaohusika na usalama. Pia kwa kuweza kwa kuweza kutumika bila uwasiwasi na bila magendo yafaa kujua kutumia muda wapewa ukitumika katika masikilizano na wote wananchi na wengineo wote wanaohusika bila tofauti na bila ujeuri. Hao wanaounga mkono nchi yetu waregeze vikwazo vyao na malalamiko yafanywa yataweza kuchunguzwa pamoja kwa kupata majawabu. Na matatizo yaliyoko yapatikana katika ratiba la kazi kasimikwa na wahuzuriaji kwenyi mkutano huu wa kisiasa. Majawabu pia yatatolewa kulingana na matukio ya majadiliano kati ya wote wanaoshurulika na ujio bora wa nchi yetu. Kwani yafaa kutegemea mawazo na mafikiri yatatolewa na raïa milioni 40 na kazi zitafanywa na mikono milioni 80. Kwani watu wakikutanana na kutoleana mawazo wataweza kujenga. Ukweli watokea katika migongano ya mawazo tu. Kwani haiwezekane nchi yetu iliyo tajiri, kanena bwana Birindwa, na ajabu iwe leo katika umaskini wa mwende mkaone. Kila aliye napato kubwa atoe mchango wake kwa kuinua uchumi na toka hapo watu kupewa kazi, maisha kuwa raïsi, siasa ya kijamii kuwa bora ummani na matunzo yatolewe kwa raïa bila ubaguzi. Ya wezekana je tule samaki toka nchi za kigeni ingawa ziwa letu Tanganyika lajaa Samaki mingi ? Yaombwa kwa kila moja awezae kutoa msaada wake awe na zamiri ya kiraïa kwakuinua siasa ya kijamii na uchumi pia kifeza na hasa kusimika usalama nchini hata kama itaombwa kutoa kiasi cha asilimia (90) cha pato. Ili raïa warudilie kazi, masomo, kupata matibabu, kuwa na vyakula na vifaa vingi ghalani aliendelea kusema ndugu Birindwa Faustino waziri mkuu wa Jamhuri ya Zaïre, mzaliwa wa jimbo la Kivu ya Kusini.

André Bisimwa L-B. Tserou

UHARIRI

# Dolari kwenyi mlingoti

Hali ya kiuchumi iliyoko nchini yatia raïa katika uwasiwasi kwani hawajui nani wategemea ao nani atawaokoa na kuwaondoa katika shimo la magumu wagandamizwa. Siku kwa siku bei ya vitu hupandishwa wasijue kweli kisa cha mwendo wachukua bei sokoni, madukani na mengineo mahali. Uchumi wazorota nchini kwa jumla na mjini Bukavu kwa upekee na kando kando. Jawabu kwa tatizo hilo la kupandishwa kwa bei litoke wapi ? Wote wanaohusika watupiana lawama, viongozi wa serkali, wachuuzi kama vile wanunuzi.

Lakini jambo moja latisha mjini ni kuona bei zasimikwa kuambatana na samani ya dolari kulingana na mabadilisho yake kwa feza ya Zaïre, Rwanda ao Burundi nchi ambazo zapakana na zahusiana kiuchumi. Na hata wamama wachuuzi wa rejareja kama vile hao wa mboga, lengalenga, sombe, kuni na kazalika waeleza eti wasimika bei kulingana na samani ya dolari. Hawa husema bila kusita : "ni ninyi tu hamujue kama dolari imepanda samani ? Kumbe musishangae kama bei imepanda ". Lakini pia ni kuona hata dolari ishuke samani (valeur) bei ya vitu haiwezi kushuka bali yapanda kama mshale. Ni hapo wakaaji halaumu, huhukumu "dolari" na hulalamika itiwe kwenyi mlingoti (potence), itungikwe bila huruma.

Tukichungua kwa karibu jambo hilo, imevumbuliwa kuwa kwapatikana nchini na hasa hapa mjini Bukavu dolari za kiamerikani za uongo pia nchini Rwanda na Burundi. Na hata zaingizwa nchini mwetu kimagendo. Siyo uwongo. Kwani hata mtaalam moja mzungu toka Amerika ameweza kuhakikisha jambo hilo na kulikamilisha baada ya kuvumbua dolari hizo hapo Cyangugu kwa mrugaruga moja aliyetaka kumbadilisha feza. Mzungu huyo kazichukuwa kalazimisha wamrudishie za kwake zilizo za kweli; Kuona hivyo na baada ya kumshtiwa myangunyangu huyo, huyo kaona ni vema afyatuke bila kuomba la mwisho akiogopa mashaka yalikuwa yakimgojea. Malalamiko kazaa yasikilika punde zote mjini Bukavu. Na ni hatari uchumi upate matatizo mengi. yajulishwa pia kuwa dolari hizo za uongo zaletwa jimboni na wafanyabiashara wengi toka majimbo jirani nchini ambao wakuja kununua hasa vyakula kama vile, samaki, ndagaa, mhogo, maharagi na vinginevyo vifaa.

Kwa ngambo yao, wamama wafanyabiashara wapinga kweli wanunuzi watoka majimbo mengine na ambao wajiruhusu kuchukua vyakula na vifaa kazaa wakivinunua kwa bei kali wasimika wenyewe na ambazo zalingana mara mbili ao tatu na bei kamili. Na upungufu wa vyakula na vinginevyo vifaa wajionya sokoni kama vile madukani. Toka hayo, akina mama wachuuzi waomba kwa viongozi, wakuu serkalini na wote wanaohusika pia wakaaji wafanye vyote wawezavyo jambo hilo la kitisho lipingwe na kupigwa marufuku. Na hiyo kutokana na dolari za uwongo zatolewa.

Kwa upande mwengine, yasemekana kuwa "wa Kadhafi" wa *huko Panzi* mtaani Ibanda ambao wategemea *mabadiliko nchini wanena kuwa ni* wafanyabiashara hasa wachuuzi wa zahabu *wataka kuwachonganisha na* kuwapambanisha katika *migongano na "Wana-Kasaï". Wakisema kuwa ni* "Wana-kasaï" *ndio msinji wa njaa yatezamiwa kuangamiza mji wa Bukavu.* Pia wachuuzi hao wa zahabu kutokana na hali ya kiuchumi na ya kisiasa iliyoko nchini kwa sasa wabadilisha feza za Zaïre kwa dolari na kupandisha bei ya vitu. Na feza za kigeni ndizo zafaulu kupunguza samani ya zetu "Zaïre". Wa "kadhafi" hao waomba : eti kila mwana-Zaïre, toka jimbo lolote, aje akauze vifaa ataka mjini Bukavu, wachuuzi wa zahabu na wengineo wabadili feza waache kuchochea moto wa chuki na ubaguzi wa kikabila, shirika la "Aneza" na wanawake mkusanyike kuhusu jambo hilo ili kutoa mwanga kamili kwa watu wote na kutoa shurulisho kwa tatizo hilo, eti "dolari za wana-Kasaï" ambazo wanazo wachuuzi wa zahabu na wanunuzi na wengineo wabadili feza nyumbani mwao waziweke kwenye mabenki inazo lazima, hao wanao madaraka ya kuchukua hatua na makusudio wasikie malalamiko yetu na walinde raïa, wameendelea kusema wa "kadhafi".

Toka maoni hayo, twazani kama raïa hasa wakaaji mjini Bukavu kama hawafungue macho, watatekwa nyara na kutumbukia katika mtego wa watenda maovu walio wachuuzi ama wafanyabiashara wa uwongo walio, kwa kweli, wizi watakao kuwinia miongoni mwa ndugu zao. Na kuzorotesha uchumi nchini.

André Bisimwa L-B. Tserou

# Birindwa wa UDPS ni yuda ?

***Kuhusu bwana Faustin Birindwa, gazeti JUA kapendelea kujulisha kwa wasomaji wake yale yasemwayo na vijana wa BBC/Carrefour, mtaani Kadutu pa Bukavu. Ndugu P.M. ambaye ni prezidenti wa "Buholo Businessmen, Carrefour" (BBC) atoa maoni yake:***

JUA: Yajulikana kama hapa kunako "Carrefour" mwasema mengi kuhusu siasa ya nchi. Mwaweza kutueleza machache mujuayo kuhusu bwana Faustino Birindwa ?

P.M. : Ni kweli kama twazungumza mengi kuhusu siasa, siyo tu ya Zaïre bali ya nchi mablimbali kusudi ya kupasha wengine na kutafuta jawabu la kuondoa nchi katika maangamizo iliyomo. Mpango huo ungetolewa na raia kama vile sisi, ingelikuwa jambo la kufurahisha sana.

JUA : Ni kweli kama kuna mgawanyiko wa wanamemba katika chama cha UDPS ?

P.M. : Ni bora nikujulishe kama mimi si mwanasiasa ao mwanamemba wa chama chochote. Ila kwa hali yangu ya kijana apendae mabadiliko, ningejibu kama sione kabisa mabadiliko katika chama hicho. Ikiwa mabadiliko yako ao yatukuwa, ni sababu ya bwana Biringanine na mwenzie Faustino Birindwa wapendeleao kuunda chama kingine cha siasa badala ya UDPS ambacho twajua ni kimoja na kisichogawanyika kwa vile si mali ya mtu binafsi.

JUA : Mulionaje wakati wakuu ao viongozi wa UDPS/S-K kapendelea kufanyike maandamano juu ya kutetea bwana Birindwa ili abaki katika UDPS?

P.M. : Maandamano hayo hayakuwa na maana yoyote, kwa vile ilikuwa vema kupata ukamilisho wa mabo tokea mjini Kinshasa, pahali pa kufanya kwa haraka. Lakini twajua kama bwana Birindwa na bwana Mobutu waendesha uhusiano wao tangu zamani na hata yawezekana kama urafiki wao watokana na hali hiyo. Na ni kwali kujua kama katika siasa, "morale" ya mtu yauzwa. Waonaje wewe?

JUA : Kwa nini vijana wa UDPS mjini Bukavu kaona bwana Birindwa kawa vile shetani mbele ya kujua ukweli wowote kuhusu jambo lile ?

P.M. Ikiwa vijana kamuona kama vile shetani ni sababu yeye na bwana Tshisekedi walikuwa pamoja na kuungana kweli. Wakati Birindwa kaanza kuungana na Mobutu, aliyetapikwa na wakaaji wa "Sud-Kivu", kwa kumgombeza bwana Tshisekedi, ni sherti aonekane kama vile Yuda aliye muuzisha Yesu. Bila kuenda mbali, matumikio ya Tshisekedi kapendeza watu wote. Kwa wakati huo Birindwa kaenda kinyume na mapenzi ya wakaaji wa Kivu ya Kusini, asiwaze kama anao watu nyuma yake na asijisifu wala kudanganyika kama kafanya hayo kwa jina la "Sud-Kivu". Hata kidogo. JUA : Ikiwa UDPS yapoteza mabingwa kama Birindwa na wengine, nini yaweza katokee ?

P.M. : Ni kwali kama UDPS ilikwisha poteza bwana Birindwa. Lakini ndani ya nchi si lazima kuwa na mabingwa wawili. Hata ikiwa watu na nia mbaya waweza wakamua Tshisekedi bingwa wetu, sherti mwengine ataonekana kuwa mpinzani na pambano litaendelea.

JUA : Sababu gani mwapendelea sana cham cha UDPS kuliko vinginevyo, hasa bwana Tshisekedi kuwa yeye tu aweza kuleta mabadiliko rasmi katika viungo vya serkali ?

P.M. : Nilikuambia wazi kama mimi si mwanasiasa ao mwanamemba wa chama chochote. Kuhusu UDPS, ni vizuri kuunga mkono chama hicho kwa vile kazaliwa ao kaundwa nchini wakati ambako mtu yeyote hangeweza kutoa oni lililo mbalimbali na lile la mkuuana chama aliyekuwa pia raïs wa jamhuri. Ubaya ni kuona kuwa bwana Mobutu hapendi kusikilizana na Tshisekedi ambaye kaonyesha kutumikia nchi pahali pa Mobutu apendelea kutumika na waziri mkuu atakayeiba mali ya serkali kama yeye na kumuogopa afanyapo makosa. Lakini sababu Tshisekedi hana tabia hiyo, haoni mafaa yoyote ya kutumika naye. Ila yeye pia ajue kama raïa hawapendi tena aongoze inchi.

Na Mutungwa Abandelwa Phély